

## UMUHIMU WA MISITU YA MILIMA YA ULUGURU

**Vyanzo vya maji:** Misitu ya Milima ya Uluguru ni rasilimali muhimu sana kwa maisha ya Watanzania na maendeleo ya taifa letu na dunia kwa ujumla.

Misitu ya Milima ya Uluguru ni vyanzo cha maji, mojawapo ukiwa mto Ruvu. Maji yanayotoka katika misitu hii ni muhimu kwa shughuli mbali mbali za nyumbani, viwandani, mashambani na ufugaji

**Bioanuai:** Misitu ya Milima ya Uluguru ni makazi muhimu ya bioanuai. Zipo bioanuai nyingi na za kipekee ambazo hupatikana katika hii misitu tu, mfano *kurumbizi* na *chozi moro* n.k. Misitu ya Milima ya Uluguru ina miti ya kipekee duniani aina nane kwa mfano *Mkani*.

**Hali ya hewa safi:** Misitu ya Milima ya Uluguru huleta hali ya hewa nzuri. Misitu hurekebisha hali ya hewa ikiwa ni pamoja na kuleta oksijeni angani.

**Chanzo cha Mvua:** Misitu ya Milima ya Uluguru ni chanzo cha mvua. Mvua husaidia kukuza na kuendeleza shughuli za kilimo na kuongeza chakula na kipato cha wananchi wanaozunguka maeneo ya Milima hii.

**Dawa za asili:** Misitu ya Milima ya Uluguru ni chanzo cha dawa za asili.

**Chakula:** Misitu ya Milima ya Uluguru hutupatia mazao ya msitu kama vile uyoga, matunda na mboga mboga.

- Fikiria kwanza kabla ya kuchoma moto
- Moto ni adui wa misitu na mazingira
- Epuka moto ovyo kuokoa maisha
- Sema hapana kwa moto ovyo
- Moto ovyo ni adui wa maendeleo

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:  
**Mkurugenzi Mtendaji**  
Shirika la kuhifadhi misitu ya asili  
Tanzania  
S.L.P. 23410  
Simu: +255 (0)22 2669007  
Fax: +255 (0)22 2669007  
Barua pepe: [tfcg@tfcg.or.tz](mailto:tfcg@tfcg.or.tz)  
Dar es Salaam



## HIFADHI MISITU YA MILIMA YA ULUGURU

## EPUSHA MOTO KATIKA MISITU YETU

Tuepuke kuchoma moto Milima ya Uluguru ili kunusuru vyanzo vya maji, bioanuai na kuongeza kipato



Tanzania Forest  
Conservation Group  
Kikundi Cha Kuhifadhi  
Misitu ya Asili Tanzania

## VISABABISHI VYA MIOTO:

**Uwindaji haramu:** Katika Milima ya Uluguru wawindaji huchoma moto ili kuwapata wanyama kama ndezi, panya, nguruwe pori kwa ajili ya kitoweo.

**Usafishaji mashamba:** Wakulima husafisha mashamba yao kwa ajili ya kilimo kwa kutumia moto. Hii ni tabia mbovu ya uvivu. Moto kutoka mashambani huenda hadi katika misitu na kusababisha hasara kubwa.

**Mila na jadi:** Katika maeneo mengi ya Milima ya Uluguru kuna imani kuwa usipochoma moto mvua hazitanyesha. Hivyo wakazi wa maeneo haya huamini ni vema kabisa wakati wa kiangazi wachome moto ili mvua zinyesha. Vile vile kuna imani kuwa mtu akichoma moto ukaenda mbali au ukaunguza eneo kubwa basi ataishi muda mrefu. Hizi ni imani potofu.

**Uelewa mdogo:** Wakazi wengi wa Milima ya Uluguru wana uelewa mdogo wa uhifadhi, hivyo uharibifu wa mazingira ni mkubwa likiwepo suala la uchomaji moto.

**Kujifurahisha:** Wananchi wengine huchoma moto kwa ajili ya kujifurahisha tu.

**Uvutaji sigara:** Wavutaji sigara wanachangia kusababisha moto ovyo.

**Ulevi:** Wakati wa usiku walevi huchoma moto ili waweze kuona njia vizuri kwa sababu ya giza

**Wafugaji:** Wafugaji huchoma ili majani machanga yatokee ili mifugo yao ipate lishe. Wafugaji huthamini zaidi mifugo yao bila kujua kuwa uharibifu wa moto ni mkubwa

**Usalama:** Kufukuza wanyama wakali wasije karibu na makazi. Wakazi wa Milima ya Uluguru wanaoishi karibu na misitu huchoma moto ili kufukuza wanyama

## MADHARA YA UCHOMAJI MOTO OVYO KATIKA MISITU YA MILIMA YA ULUGURU

**Kuharibu uoto wa asili:** Uoto wa asili huaribika

**Mabadiliko ya hali ya hewa:** Kuchoma misitu huchangia kuongezeka kwa hewa ya ukaa(Co<sub>2</sub>) angani. Misitu ni nguzo muhimu ya kuondoa hewa ukaa katika anga. Kuendelea kuwepo hewa ukaa husababisha mabadiliko ya hali ya hewa (climate change) ambayo ni pamoja na ongezeko la joto.

**Uharibifu wa bioanuai:** Uchomaji wa misitu hupunguza bioanuai za kipekee katika Milima ya Uluguru ambazo huvutia watalii.

**Umasikini:** Uchumi kuharibika na hivyo kuongezeka kwa umaskini

**Upungufu wa maji:** Uchomaji moto husababisha upungufu wa maji kwani vyanzo vya maji huharibiwa.

**Vifo:** Moto husababisha vifo



## TUFANYE NINI KUONDOA TATIZO LA MOTO KATIKA MILIMA YA ULUGURU?

**Wananchi:** Kila mkazi wa maeneo ya Milima ya Uluguru achukue tahadhari wakati wa kutumia moto na kulaani vikali vitendo vya kuchoma moto misitu, mapori na nyika



**Elimu:** Elimu ya uhifadhi inahitajika kwani iliyopo hitoshi.

**Sheria:** Vijiji vitunge sheria ndogo za mazingira. Sheria mama zilizopo zinatakiwa zitumike na zisisitizwe.

**Vyombo vya habari:** Vyombo vya habari kama radio, luninga, magazeti, mabango, vipeperushi vitumike kuelimisha jamii.

**Kamati za moto:** Kila kijiji kianzishe kamati za kuthibiti moto (fire patrols)

**Ufugaji:** Kupata kitoweo mbadala kwa kuhimiza ufugaji wa kuku, mbuzi na wanyama wafugwao.

**Elimu ya jadi:** Itumike hasa sehemu ambapo ina kipaumbele

**Matumizi ya ardhi:** Vijiji vinahitaji kuwa na utaratibu mzuri wa matumizi bora ya ardhi (land use plans). Familia zimilikishwe ardhi kisheria.